

CHRISTADELPHIAN HYMN BOOK
FOR WORSHIP AND FOR WITNESS

*“I will praise thee with my whole heart: before the gods
will I sing praise unto thee. I will worship toward thy holy temple and
praise thy name for thy loving kindness and for thy truth: for thou hast
magnified thy word above all thy name” Psalm 138:1,2*



KITABU CHA NYIMBO ZA NDUGU KATIKA KRISTO
CHA KUABUDU NA USHUHUDA

*“Nitakushukuru kwa moyo wangu wote, mbele ya miungu nitakuambia
zaburi. Nitasujudu nikilikabili hekalu lako takatifu, nitalishukuru jina
lako, kwa ajili ya fadhili zako na uaminifu wako, kwa maana umeikuza
ahadi yako, kuliko jina lako lote” Zaburi 138:1,2.*

Eighth (9th) Edition

Reprinted March, 2023

HOW TO PRESIDE BREAKING OF BREAD MEETING & USE OF HYMNS

Introduction

Presiding is very important. A good president can set a spiritual tone for the meeting, compliment the exhorter with prayers and hymns that link in with his theme, and bring brothers and sisters to meet the Lord Jesus in the bread and the wine.

Preparation

Be well prepared, be thoughtful, and start on time. An unprepared president will send a message that the breaking of bread is unimportant. Pray and ask for God to help you preside well.

The exhorter will have a theme, possibly based on the daily Bible readings. If the presider's remarks together with hymns and prayers are related to the theme, the whole service will be more powerful.

Read the daily readings or any as agreed with the exhorter and pick up other themes that you can use in your comments or in prayers.

Give the Bible readers and those to lead in prayers plenty of notice so that they have time to prepare and in case they are not participating in the actual breaking of bread and taking wine they should not participate in any of the activities such as readings, prayers and serving. It has been noted where presider without prior notice calls out a brother either to read the Bible or lead in prayers or serving the emblems and collections leads to confusion as the brother might decline it in public, or does the duty as requested by the presider but either unprepared and unwillingly either participates in the emblem or does not participate in the emblem.

Welcome

Remember those brethren who are not there, perhaps they are ill, working and need a special mention, or are away travelling of visiting other ecclesias.

The presiding brother should conduct service while standing, also during singing and prayers the congregation should be standing.

Hymns

Contact the speaker before the Sunday and ask him what his theme is and whether he has any hymns that would link with his exhortation. If not, choose hymns that do support the theme in the exhortation. Try not to choose hymns that the Ecclesia does not know. Leave those hymns to another occasion or to practice. Truly, it is highly highly recommended, either on the very day of the memorial meeting or some days earlier the ecclesia or lead singers (choir) do practise the hymns to be sung on the memorial meeting.

Opening hymn should be from Psalms, Praise or Thanks to God sections of our Hymn book. Just like a prayer as taught by our Master the opening hymn should be dedicated to thank or praise God, the creator and preserver of our lives. However when given proper and benefiting introductions, some well selected hymns in Prayer and Confidence and Jesus' Ministry and the Gospel Section in this hymn book can be used in any of the hymns in Memorial meeting. There are also specific hymns for other sections in the memorial meeting.

Please it should be noted that not all hymns are purposeful in the memorial meetings but some are for other meetings like Bible studies, some at home before going to sleep among others. For example hymns numbers 189, 190 and 191 are good choice for dismissal but cannot be sang as an opening hymn in a memorial meeting nor opening Bible Study section. Just imagine how unpleasant it is the opening hymn being hymn number 179 – *Abide With Me* an evening hymn unless the breaking of bread service is being held at night.

Always pick a hymn you know the content and make sure you know it, instrumentalist(s) or someone either already appointed or usually does

it can start for you or give the music note so that you start with right or high note or voice.

Announce the number and the title of the hymn. As brethren open the hymn, read the first paragraph of the hymn or make any comments and then proclaim all to stand up before either you or any other gives the key and all start singing.

Do not pick ambiguous hymn just for the sake!

Readings

Your ecclesia will have a preference as to whether one or two or three readings are read. There is no right answer. Flexibility is often the best option. The speaker may need a reading either within the daily readings or not one of the daily readings.

Prayers

The one who utters the words in prayer does it on behalf of the rest of the congregation. With that in mind prayers should be conducted on behalf that is in plural and singular. 'Our Father' not 'my father' 'we come before you, we thank you' etc so that members in unison can conclude with Amen! That is in agreement. Remember Our Lord's prayer where Jesus did on behalf of the rest and it's in plural:

Our Father in heaven, hallowed be your name, your kingdom come, your will be done, on earth as in heaven. Give us today our daily bread. Forgive us our sins as we forgive those who sin against us.

And lead us not into temptation, and deliver us from evil.

For the kingdom, the power, and the glory are yours now and for ever. Amen.

Traditionally and it is recommended the opening prayer in a memorial meeting is led by the presiding brother. However in other Bible based meetings, any other brethren can lead. What should a president pray for?

It is a great responsibility to pray on behalf of the ecclesia. Your problems will be different from theirs, so think about the needs of the ecclesia.

A prayer that has only list of requests will not uplift the ecclesia. Again, note that the Lord's prayer and the balance between praise, thanks and requests.

This though is the main prayer of the ecclesia and many things need to be prayed for over a period of time, not necessarily every week.

Petitions could include:

- Return of Jesus
- Forgiveness
- Help for the speaker that's the exhorting brother.
- Any issues in the ecclesia
- Welfare needs
- Preaching work
- A theme coming from the speaker or the readings
- The ecclesia's activities, mission work etc.

However other prayers in the memorial meeting should focus on the issue at hand. Don't thank God for the rains or weather when giving thanks for the bread or wine. Some have used prayers as announcement where they pray on something that some or all members are not aware of and that can change the mood of the meeting.

Emblems

The bread and wine, as symbols of the life and sacrifice of Jesus, bring us to the central part of our week. It is a time for all to reflect on God's grace and their response to it. A good meeting will bring a brother or

sister to open up their hearts before God and the Lord Jesus and lead to a rededication of following the Lord.

If the speaker has already brought the meeting to think of the bread and the wine, the president does not need to repeat anything the speaker has said, nor is there a need to read verses, as minds are already focused on his sacrifice and love. The less said the better. Silence allows the meeting to concentrate their minds.

If the speaker has not mentioned about the emblems, then the president has to remind the meeting why they are here. This can be done by:

- A short comment on the death and resurrection of Jesus.
- Reading an appropriate bible passage.

Often, president reads the same bible passage (1 Cor 11.24+). Overuse of this passage leads to it being too familiar and less powerful. There are many others that could be used, such as:

- Mt 26.26
- Luke 24.30
- Isaiah 53 (many verses are appropriate)
- John 6.53

Be careful not to try and “correct” the speaker or “improve” the exhortation. This might change the theme of the exhortation.

Give thanks first before you actually break into pieces the whole bread. Newly presiding brothers tend to forget this.

Some presidents take the bread and wine before the ecclesia does, others do it last. There is no right way, but John 13 may lead presidents to take it last. Others presiding brethren hold the bread or the cup (glass) while either them or another is giving thanks which does make sense neither give any correctness.

Collections

Let collections be part of the memorial meeting as part of giving and dedications as our Lord showed. Let the presider remind the objective for collection as either for an ecclesial project or helping a family or helping in bus fares to the meetings or brethren or a project far away etc. Collections should not be done while

singing the breaking of bread hymn as it conveniences as some have to get money from their pockets, pulse, wallets etc while still holding hymn book and singing. Let there be order!

Announcements

Let the announcement be done either by the presiding brother or the ecclesial elder or any other one appointed. Announcements can be done at the beginning or at the end of the service or after collections before closure. However it is highly recommended to be done earlier before opening prayer so that some of the items can be incorporated in the opening prayer and be in brethren's minds throughout the meeting.

Summary

A good president prepares thoroughly and prayerfully. A good president selects the right hymns to edify all present and mostly to honour God and His son.

May God bless you in your work for Him.

1 Timothy 5:17: Elders who provide effective leadership must be counted worthy of double honor, especially those who work hard in speaking and teaching.

Memorial Service Program

The presiding brother to make sure all are sited and silence observed.

1. Welcome note.
2. Opening Hymn.
3. Ecclesial Announcement - either by the ecclesial elder or by the presiding brother or any other brother permitted by the elder.
4. Opening Prayer.
5. Bible Daily Readings. The ecclesial could be reading all the daily readings or some or the Exhorting brother's selected reading.
6. Exhortation.
7. Prayer for Bread.
8. Prayer for Wine.
9. Hymn for Emblems.
10. Collections.
11. Closing Hymn
12. Closing Prayer

NB: Other announcements or reactions to initial announcements can be done after closing prayer.

JINSI YA KUANDAA IBADA YA KUMEGA MKATE NA MATUMIZI YA NYIMBO

Utangulizi

Kiongozi wa ibada ni wa muhimu sana. Mwenye kiti wa ibada atamwongoza ndugu muonyaji kwa maombi na nyimbo zinazoambatana na maonyo ya siku hiyo na kuwaleta ndugu (hapa kumanisha wote wa kike na kiume) katika kukumbuka kifo cha Yesu Kristo kupitia kumega mkate na kunywa divai.

Maandalizi

Kwa kiongozi wa ibada; jiandae vyema kwa umakini na uanzishe ibada kwa muda uliopangwa. Kumbuka kwamba uongozi mbaya wa ibada

utaifanya ibada yenyewe kuwa ya kuchosha na isiyoleta umuhimu wa kumega mkate na kunywa divai. Mwombe Mungu akuongoze katika usimamizi wako wa ibada. Chukua hiyo kama nafasi maalumu, ya heshima na ya muhimu hata kama umezoa kufanya kila wakati na kila juma.

Ndugu muonyaji atakuwa na somo katika maonyo ambalo linaweza kuwa na limeambatana na vifungu vya Biblia kwa siku hiyo. Kwa hivyo kama ndugu muonyaji katika ibada ametoa somo, maombi na nyimbo viambatane na somo hilo na hivyo basi ibada nzima itakuwa ya kupendeza sana.

Soma masomo yote ya siku hiyo au somo lile Ndugu muonyaji atakalopendekeza na uchague vipengele utakavyotilia mkazo hasa katika maombi.

Kumbuka kuwajulisha mapema ndugu watakaohusika katika usomaji na maombi ili wawe na muda mwafaka wa kujiandaa na iwapo moja wao hata shiriki katika meza ya Bwana hatajiiondoa katika kufanya kazi yeyote katika hiyo ibada. Imeshaonekana wakati mwingine msimamizi wa ibada anatangaza na kumuita ndugu asome somo la Biblia au aongoze katika maombi au kutumika na huyo ndugu alikuwa amejioji na kupanga hasishiriki katika meza ya Bwana. Kwa hivyo itambidi akatae kwa umati au ashiriki akiwa hakuwa amepanga kujihuzisha au atumike na hasishiriki katika meza ambayo hayo ni makosa makubwa sana..

Jinsi ya Kuanzisha Ibada

Kanisa linastahili kuwa na furaha kwa kukutana kwa mara nyingine ili kukumbuka kifo cha Bwana Yesu Kristo.

Kwa kiongozi wa ibada; Anzisha ibada kwa toni ya juu, onyesha tabasamu, moyo wa uchangmfu na uwakaribishe ndugu na dada. Kumbuka kumtambua ndugu ambaye ni mgeni siku hiyo. Epuka kuwataja marafiki kwani ibada hii ni kwa ndugu waliobatizwa katika imani ya Kristadelfiano. Cha msingi wakaribishe ndugu na marafiki kwa ujumla na uweke wazi kuwa ibada ya kumega mkate ni kwa Ndugu na dada waliobatizwa katika imani ya Kristadelfiano. Kumbuka kuwataja ndugu waliokosa kuhudhuria, pengine kwa kukumbwa na

dharura, kazi au wametembelea makanisa mengine ya imani yetu.

Kwa kiongozi wa ibada; kumbuka kutoa maelezo yoyote ukiwa umesimama na ifikapo wakati wa maombi au nyimbo, kanisa linafaa kuwa limesimama.

Nyimbo

Kwa kiongozi wa ibada; kumbuka kuonana na ndugu muonyaji kabla ya ibada ili kujua maudhuhi ya maonyo yake na kama ameandaa nyimbo zinazoambatana na maonyo yake. Iwapo hajaandaa nyimbo zozote basi unalo jukumu la kuchagua nyimbo zinazoambatana na maonyo ya siku hiyo. Epuka kuchagua nyimbo ngeni (ambazo hazijulikani) Ni vyema nyimbo ambazo hazijulikani kuwepo na muda maalum wa kufanyia mazoezi katika kwaya hususani siku kabla ya ibada.

Nyimbo za kufungua ibada zinafaa kutoka katika kipengele cha Zaburi, Sifa na Shukrani kwa Mungu katika vitabu hiki chetu cha nyimbo. Kama ilivyo maombi vile tunavyofunzwa na Mwalimu wetu mkuu Yesu Kristo, nyimbo za kufungua ibada zinafaa kuwa za kumshukuru na kumtukua Mungu muumba na mlinzi wa maisha yetu. Hata hivyo, mwongozo ukiwa bora nyimbo kutoka sehemu za Maombi na Mwongozo, Huduma Yake na Injili katika kitabu hiki cha nyimbo zinaweza kutumika popote katika ibada nzima. Ikumbukwe pia kuna nyimbo za shughuli maalum katika ibada.

Kumbuka sio nyimbo zote zenye maana katika ibada ya kumega mkate. Nyimbo zingine hutumika katika masomo ya Biblia, nyumbani, kabla ya kulala na kadhalika. Mfano; Wimbo nambari 189, 190 na 191 ni bora zaidi kutumika kuimbwa ule muda wa kuagana au kufunga ibada wala hauwezi kuimbwa mwanzoni mwa ibada au mwanzo wa masomo ya Biblia. Hebu fikiria farakano ilivyo wimbo wa kufungua ibada ya kukumbuka kifo cha Yesu kristo ni wimbo nambari 179 – *Kaa Nami ni Usiku Tena* ambao ni wimbo wa jioni hata kama ibada inafanywa jioni.

Wakati wowote chagua nyimbo unazozijua vyema au mchezaji wa ala za muziki anafaa kuanzisha wimbo au kiongozi wa ibada aanzishe kwa toni ya juu ili wimbo uimbwe kwa ufasaha. wajulishe kanisa nambari na jina la wimbo. Wakati ndugu wanapofungua vitabu vyao vya

nyimbo unaweza kukisoma kifungu cha kwanza na kusisitiza mambo muhimu kisha unaweza kuhimiza watu wote wasimame kabla wimbo haujaanzishwa na watu wote kuimba. Epuka kuchagua nyimbo bila kujishauri.

Masomo

Kwa kiongozi wa ibada; kuna uhuru wa kusoma aidha vitabu vyote vitatu au kile ndugu muonyaji atakachopendekeza kutegemeana na wakati au desturi ya Eklesia. Ndugu muonyaji anaweza kuchagua vitabu vyote vitatu visomwe au kimoja tu katika hivyo au kutoka sehemu ingine. Ijulikane kwamba kuzingatia wakati ni jambo muhimu sana katika ibada.

Maombi

Kwa anaeongoza kwa maombi; itambulike ya kwamba anafanya hivyo kwa niaba ya kanisa zima kwa hivyo maneno yanafaa kutamkwa kwa wingi wala sio kwa umoja. Mfano: Unafaa kusema, "*Baba yetu*" wala sio, "*Baba yangu*", "*Tunakuja mbele zako*" wala sio "*Ninakuja mbele zako*", "*Tunakushukuru*" na sio "*Ninashukuru*" na kadhalika. Hii inasababisha ndugu wote kwa umoja waseme, AMEN! baada ya maombi. Kumbuka sala ya Bwana pale Yesu alipoomba kwa niaba ya wengine alitumia wingi.

Baba yetu uliye juu mbinguni, jina lako litukuzwe.

Ufalme wako na uje, mapenzi yako yatimie hapa duniani kama juu mbinguni.

Utupe leo rizki yetu, tusamehe makosa yetu kama tunavyo wasamehe wanaotukosea.

Usitutie majaribuni, bali utuokoe na yule mwovu. Kwa kuwa ufalme ni wako, nguvu na utukufu hata mulele,

AMEN.

Kama ilivyo desturi ya ibada za ndugu katika Kristo, kiongozi wa ibada anafaa kufungua ibada kwa maombi. Hata hivyo, katika mikutano mingine ya Biblia kama masomo ya Biblia, ndugu yeyote anaweza kufungua mkutano kwa maombi. Kiongozi wa ibada anafaa kuomba nini? Ana jukumu kubwa la kuomba kwa niaba ya kanisa. Kwa kuwa kila mtu anahitaji tofauti na yule mwingine, hivyo basi kiongozi wa ibada anafaa kutilia maanani mahitaji ya kanisa. Maombi

ambayo yako na mahitaji pekee hayataasisimua kanisa. Kumbuka tena mwongozo uliopo katika sala ya Bwana, kumbuka kusawazisha sifa, shukrani na mahitaji katika maombi yako. Haya ndiyo maombi makuu ya kanisa na kuna maombi mengi yanayohitajika kuombewa kwa muda wowote, sio lazima kila juma. Mambo muhimu yakuzingatia katika maombi ni:-

- Kurudi kwa Yesu Kristo
- Msamaha wa dhambi.
- Kumwomba ndugu muonyaji.
- Jambo lolote muhimu katika kanisa
- Mambo yanayohitaji ushirikiano na ustawi wa jamii
- Kuneza injili na kazi ya kuhubiri
- Maudhuhi ya masomo ya siku hiyo au kutoka kwa muonyaji
- Shughuli zote za kanisa kwa mfano kueneza injili, kuhubiri nk.

Hata hivyo maombi ya katikati ya ibada yanafaa kuzingatia yale mambo yanayoyahusu. Kumbuka sio lazima kushukuru Mungu kwa mvua au hali nzuri ya anga wakati wa maombi ya kushukuru mkate na kunywa divai. Wengine wametumia maombi kama njia ya kufanya matangazo kwa kuomba kuhusu jambo ambalo ama wote au wachache hawafahamu.

Kumbukumbu za Kifo cha Yesu Kristo

Ikumbukwe kwamba mkate na divai ni mfano wa maisha na sadaka ya Yesu Kristo hivyo basi hutuleta kwenye kiini cha ibada. Huu ndio wakati wa kila ndugu kujioji maisha yake katika kumfuata Kristo na pia kuikumbuka neema ya Mungu katika maisha yake. Ibada njema itamfanya ndugu kupeleleza moyo wake na kujikabidhi upya kwa Mungu na bwana wetu Yesu Kristo.

Kama ndugu muonyaji ashaayateka mawazo ya ndugu katika kumkumbuka Yesu Kristo kupitia mkate na divai, haina haja ya kiongozi wa ibada kuyarudia aliyoyasema ndugu muonyaji, na pia haina haja ya kuvisoma vifungu kwani kila ndugu na dada anatafakari uhusiano wake na Kristo, upendo na sadaka yake Yesu Kristo wakati huo. Ni bora kutumia maneno machache ipasavyo. Kimya kinawapa ndugu na dada nafasi ya kutafakari.

Lakini kama ndugu muonyaji amemaliza bila kugugusia mkate wala divai, basi kiongozi wa ibada analo jukumu la kuwakumbusha ndugu kiini cha kukumbuka kifo cha Yesu Kristo na sababu juu ya kuula mkate na kukinywea kikombe. Hili linaweza kukelezwa kupitia:

- Maelezo mafupi ya kufa na kufufuka kwa Yesu Kristo.
- Kusoma kufunga mwafaka.

Mara nyingi viongozi wa ibada wamekuwa wakisoma kifungu kimoja tu (1 Wakorintho 11:24+). Itambulike usomaji wa kifungu kimoja kila wakati husababisha kupoteza ladha na umuhimu wake. Vipo vifungu vingi vinavyoweza kutumika katika ibada ya kumega mkate. Navyo ni kama vile:

- Mathayo 26:26
- Luka 24:30
- Isaya 53 (misitari kadhaa)
- John 6:53

Kuna wakati kuwa mwangalifu usimkosoe ndugu muonyaji wala kuongezea maonyo yake. Jambo hili linaweza kupunguza au kubadili maudhuhi ya maonyo hayo.

Matoleo

Ifafanye matoleo yawe sehemu ya ibada na kwamba ni sehemu ya kujitolea kwa kazi ya Mungu. Kiongozi wa ibada aelezee nia ya matoleo hayo; iwapo yatasaidia miradi ya kanisa, au kusaidia familia

inayohitaji au ndugu au dada anayehitaji usaidizi. Matoleo pia yanaweza kusaidia miradi ya kanisa lililo mbali na kadhalika. Matoleo yasitolewe wakati wimbo wa baada ya kunywa divai unaimbwa kwa sababu uleta usumbufu wakati ndugu huwa wanatoa matoleo yao kwenye vibeti, mapochi na kadhalika na huku wameshikilia kitambo cha nyimbo. Kuwe na mpangilio maalum.

Matangazo

Inapendekezwa kwamba matangazo yatangazwe na kiongozi wa ibada au kiongozi wa kanisa au ndugu au dada yeyote atakayependekezwa. Matangazo yanafaa kutangazwa mwanzoni mwa ibada au baada ya matoleo kabla maombi ya kufunga ibada ndio kama kuna mambo yanahitaji maombi yatajumuishwa katika maombi ya kufungua au kufunga. Hata hivyo, inapendekezwa matangazo yawe mwanzoni mwa ibada ili mada kuu zikumbukwe katika maombi ya kufungua ibada na pia mada kuu ziwe katika mawazo ya ndugu na dada wakati wa ibada.

Maelezo Zaidi

Kiongozi bora wa ibada hujiandaa kikamilifu na kwa maombi. Pia kuchagua nyimbo zinazoambatana na maudhuhi ya maonyo ya siku hiyo na zaidi ya yote kumtukuza Mungu na mwanawe Yesu Kristo.

Mungu akubariki katika kazi unayomfanyia.

I Tim 5:17

Wazee wa kanisa wanaoongoza shughuli za kanisa vizuri wanastahili heshima mara mbili, hasa wale ambao kazi yao ni kuhubiri na kufundisha

Mfano wa Mpangilio wa Ibada ya Mkate na Divai

Ndugu msimamizi kuhakikisha wote wamekataa na kuna utulivu.

1. Kuwakaribisha.
2. Wimbo wa kufungua ibada.
3. Matangazo ya Kanisa - yafanywe na mzee/kiongozi wa kanisa au msimamizi wa ibada ama ndugu aliyeteuliwa na mzee wa ekklesia.
4. Maombi ya kufungua ibada.
5. Masomo ya Biblia ya kila siku yote au mbili au moja; au na somo kutoka kwa ndugu anaye peana neno la himizo.
6. Himizo/maonyo.
7. Maombi ya mkate.
8. Maombi ya divai.
9. Wimbo wa kukumbuka kifo cha Yesu Kristo.
10. Matoleo.
11. Wimbo wa kufunga ibada.
12. Maombi ya kufunga ibada. Exhortation.

Preface

The very first Christadelphian hymn book, *The Golden Harp*, was compiled by Robert Roberts and published in 1864, and since then new editions have appeared regularly to meet the growing needs of our community. Christadelphian hymn books in Kiswahili and English have been in use for forty years, and this latest edition expands on earlier collections, providing many more examples of hymns based firmly on the foundation of Scripture and reflecting our beliefs.

Hymns give us opportunities to express our praise, worship, petition and devotion. The act of singing together raises our spirits and brings us closer to each other in the love of Christ Jesus our Lord and the honouring of his Father and ours. The writer of a previous Christadelphian hymn book preface hoped that the chosen hymns would '*prove to be an up building and stimulating influence, and an effective help to all who desire to worship God in spirit and in truth*', and it is the prayer of the compilers of this new collection that those who use it will experience the same benefits as they prepare for the return of their Lord.

In addition to hymns and choruses previously in use many have been drawn from other sources, either in response to requests, or because the compilers themselves felt they were a worthy addition to our praise. The result is the largest and most varied collection ever available to Christadelphians in Swahili speaking regions. We hope it will strengthen our faith in "the things concerning the Kingdom of God and the name of Jesus Christ." This should be the foundation of the true worship.

Utangulizi

Kitabu cha kwanza kabisa cha nyimbo za Ndugu katika Kristo (*Kristadelfiani*) kilichojulikana kama *The Golden Harp*, kilikusanywa na Robert Roberts na kuchapishwa mnamo mwaka wa 1864, na tangu wakati huo nakala zingine zimetokea mara kwa mara kutimiza mahitaji yanayoongezeka katika jamii yetu. Vitabu vya nyimbo za Ndugu katika Kristo katika lugha za Kiwahili na Kingereza zimetumiwa kwa mda wa miaka arobaini, na nakala hii inaongezea nakala iliyopita, ikionyesha mifano mingi ya nyimbo zinazozingatia mafundisho ya msingi na kuonyesha imani yetu.

Nyimbo za Mungu utupatia nafasi ya kumtukua, kumuabudu, kuomba na kujitolea. Kitendo cha kuimba pamoja huinua roho zetu na kutuleta pamoja katika upendo wa Yesu Kristo Bwana wetu; na kutukuzwa kwa Babaye na ambaye ni Baba yetu pia. Mwandishi wa utangulizi katika kitabu cha awali cha nyimbo za Ndugu katika Kristo, alitumaini ya kuwa nyimbo zilizochoaguliwa '*zitathibitisha kuwa za kujengana na kuisisimua; na msaada wa maana kwa wote walio na hamu ya kumuabudu Mungu katika roho na kweli*'; na ni maombi ya waliokusanya hizi nyimbo ya kuwa wale watakaotumia watafaidika kama waliotangulia, wanapongojea kurudi kwake Kristo.

Kuongezea nyimbo za sifa na pambio zilipokuwa awali, nyingine zimekusanywa kutoka sehemu zingine; aidha kuitikia wale walizoziagizia au wakusanyaji walihisi ya kuwa zitakuwa za maana katika sifa. Matokeo yake ni kitabu kilicho kikubwa na chenye nyimbo nyingi kushinda chochote kile kimekuwa na ndugu wa Kristo katika maeneo yanayozungumzwa Kiwahili. Tunatumaini ya kuwa kitainua imani yetu katika "*mambo yanoyohusu ufalme wa Mungu na jina lake Yesu Kristo.*" Na huu uwe msingi wa ibada ya kweli.

YALIYOMO (CONTENT)

Zaburi (<i>Psalms</i>)	1 – 8
Sifa kwa Mungu (<i>Praise to God</i>)	9 – 34
Maombi na Mwongozo (<i>Prayer and Confidence</i>)	35 – 53
Neno la Mungu, Bibilia (<i>The Word of God, Bible</i>)	54 – 61
Yesu Kristo (<i>Jesus Christ</i>):	
Kuzaliwa Kwake (<i>His Birth</i>)	62 – 68
Kifo na Dhabihu Yake (<i>His Death and sacrifice</i>)	69 – 79
Kumega Mkate (<i>The Breaking of Bread</i>)	80 – 84
Kufufuka na Kupaa Kwake (<i>His Resurrection and Absence</i>)	85 – 92
Kurudi Kwake (<i>His Return</i>)	93 – 100
Ufalme Wake (<i>His Kingdom</i>)	101 – 113
Israeli (<i>Israel</i>)	114 – 115
Huduma Yake na Injili (<i>His Ministry and the Gospel</i>)	116 – 152
Maonyo (<i>Exhortation</i>)	153 – 173
Majira na Jioni (<i>Seasons and Evening</i>)	174 – 188
Kuachana (<i>Dismissal</i>)	189 – 191
Vijana na Watoto (<i>Youth and Children</i>)	192 – 199
Pambio (<i>Choruses</i>)	1 – 25

THE PSALMS

1. All People That On Earth Do Dwell

1. All people that on earth do dwell,
Sing to the Lord with cheerful voice,
Him serve with mirth, His praise forth tell,
Come ye before Him and rejoice.
2. Know that the Lord is God indeed,
Without our aid He did us make,
We are his flock, He doth us feed,
And for his sheep He doth us take.
3. Oh enter then His gates with praise,
Approach with joy His courts unto,
Praise, laud, and bless His name always,
For it is seemly so to do.
4. For why? The Lord our God is good,
His mercy is forever sure,
His truth at all times firmly stood,
And shall from age to age endure.

ZABURI

1. Enyi Mkaao Nchi

1. Enyi mkaao nchi,
Mwimbieni Mungu sana,
Msifuni kwa sauti,
Mbele zake mwakutana.
2. Mungu mwajua, kwani,
Aliyetuumba ndiye,
Atuchunga malishoni,
Na tu kundi lake Yeye.
3. Haya malangoni Mwake,
Hata njiani imbeni,
Mulikuze Jina lake,
Jina la Bwana si duni.
4. Bwana, Jehova ni mwema,
Ana rehema milele,
Kweli yake yasimama,
Leo na kesho vivile.

THE PSALMS

2. As Pants The Heart For Cooling Streams

1. As pants the heart for cooling streams,
When heated in the chase,
So longs my soul, O God, for thee
And thy refreshing grace.
2. For thee, my God the living God,
My thirsty soul doth pine,
Oh when shall I behold thy face,
Thou majesty divine?
3. Why restless, why cast down my soul?
Hope still and thou shalt sing,
The praise of Him who is thy God,
Thy health's eternal spring.

ZABURI

2. Kama Anavyotamani

1. Kama anavyotamani
Maji mwenye kiu,
Ndivyo ilivyo rohani
Tamaa ya wokovu
2. Uliye hai ni kwako
Roho ina kiu;
Hata lini uso wako
Utafichwa kwangu?
3. Kwa nini, moyo kuzima?
Tumaini kwake
Unywe maji ya uzima,
Wimbe sifa zake.

3. Behold, How Good A Thing It Is

1. Behold, how good a thing it is,
And how becoming well,
Together such as brethren are
In unity to dwell.
2. Like precious ointment on the head
That down the beard did flow,
E'en Aaron's beard, and to the skirt
Did of his garments go.
3. As Hermon's dew, the dew that doth
On Zion's hill descend;
For there the blessing God commands
Life that shall never end.

3. Je Kizuri Cha Ajabu

1. Je, kizuri cha ajabu
Chema cha ajabu,
Ushirikiano wa ndugu,
Umoja twaishi.
2. Kama mafuta ya kichwa
Chini ndevu ya enda,
Hata ndevu zake Haruni,
Chini nguo ya enda.
3. Kama umande wa Harmoni,
Ushukao Sayuni
Huko baraka zaa Mungu,
Agano milele.

4. O God Our Help In Ages Past

1. O God our help in ages past,
Our hope for years to come,
Our shelter from the stormy blast,
And our eternal home.
2. Beneath the shadow of Thy Throne
Thy saints have dwelt secure;
Sufficient is Thine arm alone,
And our defense is sure.
3. Before the hills in order stood, Or
earth received her frame, From
everlasting Thou art God, To
endless years the same.
4. A thousand ages in thy sight
Are like an evening gone,
Short as the watch that ends
The night Before the rising sun
5. Time, like an ever-rolling stream,
Bears all its sons away,
They fly forgotten as a dream
Dies at the opening day.
6. O God our help in ages past,
Our hope for years to come,
Be thou our guard while troubles last
And our eternal home.

4. Mungu Msaada Wetu

1. Mungu msaada wetu
Tangu miaka yote,
Ndiwe bora ngome yetu
Twakaa dawamu.
2. Kivuli cha kiti chako
Ndiyo ngome yetu,
Watosha mkono wako
Ni ulinzi wetu.
3. Kwanza havijakuwako
Nchi na milima,
Ndiwe Mungu chini yako
Twakaa salama.
4. Miaka elfu ni kama
Siku moja kwako,
Utatulinda daima
Tu wenyeji wako.
5. Binadamu huondoka
Mwisho hana kitu,
Kama ndoto hutoweka
Ndiyo hali yetu.
6. Mungu msaada wetu
Tangu miaka yote,
Ndiwe bora ngome yetu
Twakaa dawamu.

5. The King Of Love My Shepherd Is

1. The King of love my Shepherd is,
Whose goodness faileth never,
I nothing lack if I am His,
And He is mine forever.
2. Where streams of living water flow
My ransomed soul He leadeth,
And where the verdant pastures grow
With food celestial feedeth.
3. Perverse and foolish oft I strayed,
But yet in love He sought me,
And on His shoulder gently laid,
And home, rejoicing brought me.
4. In death's dark vale I fear no ill,
With Thee, dear Lord, beside me;
Thy rod and staff my comfort still,
Thy cross before to guide me.
5. Thou spread'st a table in my sight
Thy unction grace bestoweth,
And O, what transport of delight
From Thy pure chalice floweth!
6. And so through all the length of days
Thy goodness faileth never;
Good Shepherd, may I sing Thy praise
Within Thy house for ever.

5. Ni Mfalme Wa Mapenzi

1. Ni mfalme wa mapenzi
Ndiye anichungaye
Sipungukiwi, hawezi
Kunipoteza yeye.
2. Kando ya maji uzima
Yeye huniongoza,
Katika malisho mema
Daima hunilisha.
3. Mara nyingi hupotea
Kwa ukaidi wangu,
Naye huniandamia
Hunirudisha kwangu.
4. Uvulini mwa mauti
Sichi hatari kamwe,
Wewe Bwana huniachi,
Mwokozi wangu wewe.
5. Waniandalia meza,
Neema kwako tele
Kwa wewe, yote naweza,
Na msalaba mbele.
6. Kamwe hautapungua
Huo, wema wako;
Mwisho, utaniingiza,
Nyumbani niimbe kwako

6. The Lord's My Shepherd

1. The Lord's my Shepherd, I'll not want.
He makes me down to lie
In pastures green, He leadeth me
The quiet waters by.
2. My soul He doth restore again,
And me to walk doth make
Within the paths of righteousness,
E'en for His own Name's sake.
3. Yea, though I walk in death's dark vale,
Yet will I fear no ill,
For thou art with me; and Thy rod
And staff me comfort still.
4. My table Thou hast furnished
In presence of my foes;
My head Thou dost with oil anoint
And my cup overflows.
5. Goodness and mercy all my life
Shall surely follow me,
And in God's house for ever more
My dwelling place shall be.

6. Bwana Yu Mchungu Wangu

1. Bwana yu mchungu wangu,
Sitapungukiwa;
Malishoni hunilaza,
Penye utulivu.
2. Hunihuisha nafsi yangu
Pia huniongoza
Katika njia zenye haki,
Ajili ya jinale.
3. Nijapopita bondeni
Uvulini mwa kifo
Sitayaogopa mabaya,
Wewe utakuwepo.
4. Waiandaa meza yangu
Machoni pa watesi;
Mafuta umenipaka
Kikombe chafurika.
5. Kweli wema hufuata
Siku zangu zote,
Nami nitakaa nyumbani
Mwa Bwana milele.

7. O Praise Ye The Lord!

1. O praise ye the Lord,
Praise Him in the height,
Rejoice in His word, ye angels of light,
Ye heavens adore Him,
By whom ye were made;
And worship before him,
In brightness arrayed.
2. O praise ye the Lord,
Praise Him upon earth,
In tuneful accord, ye sons of new birth,
Praise Him who hath brought you,
His grace from above;
Praise Him who hath taught you,
To sing of His love.
3. O praise ye the Lord,
All things that give sound,
Each jubilant chord, re-echo around,
Loud organs His glory,
Forth tell in deep tone;
And sweet harp the story,
Of what He hath done.
4. O praise ye the Lord,
Thanksgiving and song,
To Him be outpoured, all ages along,
For love in creation,
For Eden restored;
For grace of salvation,
O praise ye the Lord.

7. Msifu Bwana

1. Msifu Bwana,
Msifu juu,
Mfurahi na, malaika juu,
E mbingu msifu,
Mlivyoubwaa;
Na mkamsifu,
Mkiangazwa.
2. Msifu Bwana,
Duniani juu,
Kwa nyimbo nzuri, m-wana wake,
Kawapa neema,
Yake msifu;
Kawapa mapenzi,
Yake msifu.
3. Msifu Bwana,
Viumbe vyote,
Shangilieni, 'kirukaruka,
Kwa matoazi,
Yavumayo sana;
Kwa kinanda sema,
Aliyofanya.
4. Msifu Bwana,
Mshukuruni,
Kwake mtoe, sauti zenu,
Alivyoviumba,
Na kuviponya;
Kwa wokovu wake,
Msifu Bwana.

8. Fill Thou My Life, O Lord, My God

1. Fill Thou my life, O Lord, my God,
In every part with praise,
That my whole being may proclaim
Thy being and Thy ways.
2. Not for the lip of praise alone
Nor e'en the praising heart,
I ask, but for a life made up,
Of praise in every part.
3. Praise in the common things of life,
In goings out and in;
Praise in each duty and each deed,
However small and mean.
4. Fill every part of me with praise,
Let all my being speak
Of thee and of Thy love, O lord,
Poor though I be, and weak.
5. So shalt Thou, Lord, from me, e'en me,
Receive the glory due,
And even now shall I begin
The song for ever new.
6. So shall no part of day or night
From sacredness be free;
But all my life, in every step
Be fellowship with Thee.

8. Nijaze Mimi Ee Mungu

1. Nijaze mimi Ee Mungu
Popote kwasifa.
Mwili wote ukutangaze
Wewe zako njia.
2. Si mdomo peke yake,
Wala moyo wasifa,
Naomba maisha yafanywe,
Popote kwa sifa.
3. Nayasifu mambo madogo,
Nikirudi nikienda.
Nayasifu na kufanya
Madogo na duni.
4. Nijaze popote kwa sifa,
Niache niseme
Wewe ni pendo Ee Bwana,
Mimi ni mnyonge.
5. Bwana kwangu nitakupa,
Utukufu na sifa.
Na sasa naimba wimbo
Kwa wewe milele
6. Mchana hata usiku,
Utukufu ujazwe.
Maisha yangu na mwendo,
Nishiriki nawe.

9. Give Thanks Unto the Lord God

1. Give thanks unto the Lord God,
He is for ever good:
His mercy lasts for ever,
He is the God of gods.
His mercy lasts for ever,
Thanks to the Lord of lords:
His mercy lasts forever,
For ever faithful, sure.
His mercy lasts forever,
For ever faithful, sure.
2. Give thanks for all his wonders,
His understanding great;
His wisdom made the heavens,
The earth and sea and sky.
He is the great Creator
Of sun and moon and stars.
His mercy lasts forever,
For ever faithful, sure.
His mercy lasts forever,
For ever faithful, sure.
3. To him who punished Egypt,
And brought out Israel;
With out-stretched arm he saved them;
He parted the Red Sea.
He overthrew the Pharaoh,
Smote other famous kings.
His mercy lasts forever,
He only does good things.
His mercy lasts forever,
He only does good things.
4. He gave the land to Israel,
Their home and heritage;
Remembered us, redeemed us,
And feeds us, Heavenly King;
Let us, then, thank our Father,
The God of heaven and earth,
His mercy lasts forever,
For ever faithful, sure.
His mercy lasts forever,
For ever faithful, sure.

9. Mshukuruni Bwana

1. Mshukuruni Bwana
Kwa kuwa ni mwema;
Kwa maana fadhili
Zake za milele.
Mshukuruni Mungu,
Bwana wa mabwana;
Kwa maana fadhili
Zake za milele.
Kwa maana fadhili
Zake za milele.
2. Afanya maajabu,
Muumba mkubwa.
Aliumba mbingu,
Nchi juu maji.
Na mianga mikubwa
Jua, mwezi, nyota
Kwa maana fadhili
Zake za milele.
Kwa maana fadhili
Zake za milele.
3. Aliwapiga Misri,
Kuwatoa Israeli.
Kwa mkono wa nguvu
Akagawa Shamu.
Akazamisha Farao
Na pia wafalme
Wenye sifa na nguvu.
Ye' ufanya mema
Kwa maana fadhili
Zake za milele.
4. Akawapatia nchi;
Uriithi wa Israeli.
Aliyetukumbuka
Pia kutuponya.
Kila chenye uhai
Akipa chakula.
Kwa maana fadhili
Zake za milele.
Kwa maana fadhili
Zake za milele.

10. O Lord Of Heaven And Earth And Sea

1. O Lord of heaven and earth and sea,
To Thee all praise and glory be,
How shall we show our love to Thee,
Who givest all.
2. The golden sunshine, vernal air,
Sweet flowers and fruit, Thy love declare,
When harvests ripen, Thou art there,
Who givest all.
3. For peaceful homes and healthful days,
For all the blessings earth displays,
We owe Thee thankfulness and praise,
Who givest all.
4. Thou didst not spare Thine only son,
But gav'st him for a world undone,
And freely, with that blessed one,
Thou givest all.

10. Bwana Wa Mbingu Na Nchi

1. Bwana wa mbingu na nchi,
Twakwinulia sauti;
Watoto wako huachi
Kuwalisha.
2. Kwa hii nuru ya jua,
Matunda mema, maua;
Kwa mavuno twatambua
Wema wako.
3. Kwa nyumba zenye salama,
Kwa afya na uzima
Na neema zote njema,
Twakusifu.
4. Mwanao umemtoa
Kuja kwetu kutufia;
Tena naye vyote pia
Umetupa.

11. O Worship The King All Glorious Above

1. O worship the King all glorious above;
And gratefully sing His power and His love;
Our shield and defender, the ancient of days,
Pavilioned in splendour, and girded with praise.
2. O tell of His might, O sing of His grace,
Whose robe is the light, whose canopy space.
His chariots of wrath the deep thunder clouds form,
And dark is His path on the wings of the storm.
3. This earth, with its store of wonders untold,
Almighty, Thy power hath founded of old;
Hath 'stablished it fast by a changeless decree,
And round it hath cast, like a mantle, the sea.
4. Thy bountiful care what tongue can recite?
It breathes in the air, it shines in the light;
It streams from hills, it descends to the plain,
And sweetly distils in the dew and the rain.
5. Frail children of dust, and feeble as frail,
In Thee do we trust, nor find Thee to fail;
Thy mercies how tender, how firm to the end,
Our Maker, Defender, Redeemer and Friend.
6. O measureless might, ineffable love,
While angels delight, to hymn Thee above;
Thy humbler creation, though feeble their lays,
With true adoration, shall sing to Thy praise.

11. Na Tumwabudu Huyo Mfalme

1. Na tumwabudu huyo Mfalme,
Sifa za nguvu zake zivume,
Ni ngao, ni ngome, yeye milele,
Ndizo sifa zake kale na kale.
2. Hubirini ya uweza wake
Mkaziimbe neema zake;
Gari yake ndiyo mawingu nayo
Nuru ni mavazi ayavaayo.
3. Tazameni u-limwengu huu
Ulivyoubwa, ajabu kuu;
Sasa umewekwa mahali pake,
Hata utimize majira yake
4. Kwa ulinzi wa-ko, kwetu Bwana,
Twakushukuru, U mwema sana;
Huwapa chakula kila kiumbe,
Kila kitu kina mahali pake.
5. Wanadamu tu wanyonge sana,
Twakutumai-ni Wewe, Bwana;
Kamwe haupungui Wako wema,
Mkombozi wetu, Rafiki mwema.
6. Uweza wako haupimiki,
Mapenzi yako hayasemeki;
Na ulivyoumba vyote kabisa,
Vidogo, vikumbwa, vyakutukuza

12. Praise My Soul The King Of Heaven

1. Praise, my soul, the King of Heaven,
To his feet thy tribute bring.
Ransomed, healed, restored, forgiven,
Evermore His Praises sing.
Praise Him, Praise Him,
Praise Him, Praise Him,
Praise the Everlasting King.
2. Praise him for His grace and favour
To our fathers in distress,
Praise Him still the same as ever,
Slow to chide and swift to bless.
Praise Him, Praise Him,
Praise Him, Praise Him
Glorious in His faithfulness.
3. Father-like He tends and spares us,
Well our feeble frame He knows
In His hands He gently bears us,
Rescues us from all our foes
Praise Him, Praise Him,
Praise Him, Praise Him,
Widely as His mercy flows.
4. Angels in your hosts adore Him;
Ye behold Him face to face;
Saints triumphant, bow before Him,
Gathered in from every race.
Praise Him, Praise Him,
Praise Him, Praise Him,
Praise ye all the God of grace.

12. Nimsifu Mungu Wangu

1. Nimsifu Mungu wa-ngu,
Amenipa furaha;
Nimepozwa, ni salama,
Atatoa wokovu.
Asifiwe,
Asifiwe,
Anipaye baraka.
2. Msifu alitete-a
Watu wakionewa;
Nimsifu hwendelea,
Kunipenda na kwombwa.
Asifiwe,
Asifiwe,
Ndiye wa kwaminiwa.
3. Kama Baba hutuli-nda,
Atujua na hali;
Hutushika tukienda,
Hufukuza wakali.
Asifiwe,
Asifiwe,
Kwa karibu na mbali.
4. Wamsifu Malai-ka,
Humtazama Bwana,
Na sisi tukifufuka
Nao tutafanana.
Asifiwe,
Asifiwe,
Yuna neema sana.

13. Praise O Praise Our God And King

1. Praise O praise our God and King,
Hymns of adoration sing,
For His mercies still endure,
Ever faithful, ever sure.
2. He with all commanding might
Filled the new-made world with light,
And the golden-tressed sun
Caused all day his course to run.
3. Horned moon to shine by night
Mid her spangled sisters bright;
Angels hosts to work His plan,
Leading onwards up to man.
4. He His chosen race did bless
In the barren wilderness.
All things living He doth feed,
His full hand supplies their need.
5. Let us, then, with gladsome mind,
Praise the Lord for He is kind;
For His mercies still endure,
Ever faithful, ever sure.

13. Mungu Na Tumsifu

1. Mungu na tumsifu
Ni Bwana mtukufu,
Na rehema vivile
Hatukosi milele.
2. Ameliumba jua,
Ndiye mleta mvua,
Akiba ya ghalani
Imetoka mbinguni.
3. Mwezi pia ni wake,
Nyota ni taa zake,
Kazi ya malaika
Nikutusaidia.
4. Ndiyo sana baraka
Kuivisha nafaka;
Majira ya mavuno,
Hutulisha vinono.
5. Sifa zako zivume,
Siku zote mfalme
Na rehema vivile
Hatukosi milele.

14. The Earth Doth Her Creator Praise

1. The earth doth her Creator praise,
And with the voices she doth raise
A wondrous harmony displays,
And we would praise Thee too.
2. She blends the sound of wind-swept trees,
Sweet songs of birds and hum of bees,
With gentlest sigh of summer seas,
And we would praise Thee too.
3. And as we in Thy love rejoice,
May each aspire with eager voice
To render music of Thy choice,
That we may praise Thee too.

Can be sang as hymn number 2 & 76

14. Nchi Iletayo Sifa

1. Nchi iletayo sifa,
Na sauti yenye sifa,
Papendezapo popote,
Tumsifu si sote.
2. Sauti nzuri ya miti,
Wimbo wa ndege na nyuki,
Bahari hari vyatoka,
Tumsifu si sote.
3. Tukifurahi pendoni,
Nasi twimbe kutamani,
Chagua wimbo moyoni,
Tumsifu si sote.

15. All Creatures Of Our God And King

1. All creatures of our God and King,
Lift up your voice and with us sing
Alleluia, Alleluia!
Thou burning sun with golden beam,
Thou silver moon with softer gleam:

*O praise Him, O praise Him!
Alleluia, Alleluia, Alleluia!*

2. Thou rushing wind that art so strong,
Ye clouds that sail in heaven along
O praise Him, Alleluia
Thou rising morn, in praise rejoice,
Ye lights of evening, find a voice:
3. Thou flowing water, pure and clear,
Make music for thy Lord to hear,
Alleluia, Alleluia!
Thou fire so masterful and bright,
That givest man both warmth and light:
4. Dear mother earth, who day by day
Unfoldest blessings on our way,
O praise Him, Alleluia!
The flowers and fruits that in thee grow,
Let them His glory also show:
5. And all ye men of tender heart,
Forgiving others take your part,
O sing ye, Alleluia!
Ye who long pain and sorrow bear
Praise God and on Him cast your care:

15. Viumbe Vya Mungu Wetu

1. Viumbe vya Mungu wetu
Mwimbieni nyimbo zetu
Aleluya, Aleluya!
Ewe jua uwakao
Na mwezi uangazao:

*Msifuni Msifuni
Aleluya, Aleluya, Aleluya*

2. Upepo unaovuma,
Mawingu juu mbinguni,
Msifuni, Aleluya l
Asubuhi msifuni,
Jioni mfurahini:
3. Maji yatiririkao,
Yamwimbie Mungu wake,
Aleluya, Aleluya!
Moto unaoangaza,
Watupa joto na nuru:
4. Dunia ni mama yetu,
Utuonyesha baraka,
Msifuni, Aleluya!
Maua unayokuza,
Utukufu muonyeshe:
5. Watu wenye myoyo safi,
Wasameheni wenzenu,
Mwmbieni, Aleluya!
Mnao zijua shida,
Mungu tegemeo lenu:

16. Immortal, Invisible, God Only Wise

1. Immortal, invisible, God only wise,
In light inaccessible hid from our eyes;
Most blessed, most glorious, the ancient of days,
Almighty, victorious, Thy great name we praise.
2. Unresting, unhasting, and silent as light,
Nor wanting, nor wasting, Thou rulest in might;
Thy justice like mountains high soaring above,
Thy clouds which are fountains of goodness and love.
3. To all life Thou givest, to both great and small:
In all life Thou livest, the true life of all;
We blossom and flourish as leaves on the tree,
And wither and perish; but nought changeth Thee.
4. Great Father of glory, pure Father of light,
Thine angels adore Thee, all veiling their sight;
All laud we would render: O help us to see,
'Tis only the splendour, of light hideth Thee.

16. Yu Hai Humuoni

1. Yu hai humuoni, Mungu mkuu,
Nuru yake hatu-wezi kuona; 'Baraka,
Mtukufu, Mzee wa siku, Mkuu,
Mshindi, twakutukuza
2. Mtulivu mpole, kama mwangaza,
Ujenga utawala, si m-hitaji
Kama milima juu, hukumu yake,
Mawingu ishara, ya wema wake.
3. Vyote umevipa, uhai wako,
Kwa kweli vyaishi, uhai wako,
Twanawiri kama, miche ya miti,
Twakauka nawe, ubadiliki.
4. U Baba mtukufu, Baba wa nuru,
Malaika wako, wakuabudu,
Kwa nguvu twaomba, tusaidie,
Tuone nuruyo, ikufichayo.

17. Thy Goodness, Lord Our Souls Confess

1. Thy goodness, Lord, our souls confess,
Thy mercy we adore-
A spring whose blessings never fail,
A sea without a shore.
2. Sun, moon and stars Thy love attest
In every golden ray;
Love draws the curtain of the night,
And love brings back the day
3. Thy bounty every season crowns
With all the bliss it yields
With joyful clusters loads the vine;
With strength'ning grain, the fields
4. But chiefly Thy compassion, Lord,
Is in the gospel seen;
There, like a sun, Thy mercy shines
Without a cloud between.

17. Wema wa Bwana Twakiri

1. Wema wa Bwana twakiri,
Huruma twabudu,
Barakazo hazikomi,
Ni kama chemchemi.
2. Jua mwezi, nyota leta,
Mapenzi ya Nuru,
Yanatuletea giza,
Kurudisha nuru.
3. Mavuno yako mwakani
Yajaa makondeni,
Matunda umeyajaza,
Mbegu mashambani.
4. Huruma zako Bwana kuu,
Katika injili,
Hapo zako ni rehema,
Wazi kama myali.

18. The God Of Abraham Praise

1. The God of Abraham praise,
Who reigns enthroned above,
Ancient of everlasting days,
And God of Love.
We worldly aims forsake,
The glory, fame and power;
And Him our only portion make
Our shield and tower.
2. Though nature's strength decay,
And all on earth withstand,
We to the Kingdom urge our way
At His command;
Our pilgrimage we pass
With Jesus in our view,
And through this dreary wilderness
Our way pursue.
3. The ransomed earth we see
With peace and plenty blest;
And there in glorious liberty
Its hosts find rest.
There milk and honey flow,
And oil and wine abound,
And trees of life for ever grow
With mercy crown'd.
4. Here dwells the Christ, our King,
Our Lord, our Righteousness;
Triumphant o'er the world and sin,
The Prince of peace;
On Zion's sacred height
He David's throne mountains,
And glorious with the saints in light-
He lives and reigns.
5. To God who reigns on high
The Seraphim all sing,
And "Holy, holy, holy" cry
"Almighty King!"
Who was, and is the same,
And evermore shall be:
O Yahweh, God of hallowed Name,
We worship Thee.

18. Mungu Wa Ibrahim Twakusifu

1. Mungu wa Ibrahim
Twakusifu huko juu,
Mungu wa upendo
Mzee wa siku.
Ya ulimwengu yote,
Na nguvu twawacha,
Wewe ni sehemu yetu
Ngao, ngome.
2. Dunia nguvu zake
Zote zadumu humu,
Sisi wake ufalme
Tunaelekea;
Safarini yetu,
Yesu Jemedari,
Kati ya jangwa hatari
Twapitia.
3. Dunia hiyo
Tutakayo ona,
Amani yake na baraka
Zimejaa
Maziwa, asali,
Mafuta ni mengi,
Miti ya uzima, hapo
Ni salama.
4. Hapo yupo Kristo,
Mfalme wa Haki
Mshindi wa ulimwengu,
Bwana wa amani;
Ameteki Zayuni, enzi ya Daudi,
Mtukufu wateule,
Watawala.
5. Kwa Mungu wetu juu,
Malaika waimba,
"Mtakatifu, Mtukufu
Mungu Mkuu"
Ndiye yeye yule,
Leo na milele,
Yahweh jina la pekee,
Twamwabudu

19. Jehovah Dwells Alone

1. Jehovah dwells alone,
No equal can He see;
Th'unchangeable and mighty God
From all eternity.
2. Through realms of boundless space
His spirit works His will;
